



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA



HALMASHAURI YA WILAYA YA KALIUA

Simu: +255262965679, +255262965676, +255622225618

Barua pepe: ded@kaliuadc.go.tz

Tovuti: www.kaliuadc.go.tz

S. L. P 83

Kaliua Tabora

KDC/M.2/VOL III/0056/18

16/11/2021

**TANGAZO LA NAFASI YA KAZI YA MSAIDIZI WA HESABU
DARAJA LA II YA MKATABA WA MWAKA MMOJA**

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua anawatangazia Wananchi wote wenye sifa kuomba nafasi za kazi ya Msaidizi wa Hesabu Daraja la II ya mkataba wa mwaka mmoja kwa wote wenye sifa kama ifuatavyo:-

MSAIDIZI WA HESABU DARAJA LA II (NAFASI 1)

1. Sifa za Mwombaji

Awe na cheti cha Astashahada ya Uhasibu kutoka Chuo kinachotambulika na Serikali au cheti cha ATEC I kinachotolewa na NBAA au sifa nyingine zinazolingana na hizo zinazotambulika na NBAA

2. Kazi za kufanya

- i. Kuandika na kutunza "register" zinazohusu shughuli za Uhasibu.
- ii. Kutunza kumbukumbu za hesabu
- iii. Kupeleka barua/nyaraka za Uhasibu Benki
- iv. Kufanya kazi nyingine za fani yake atakazopangiwa na Mkuu wake wa kazi.

MASHARTI YA JUMLA

- i. Mwombaji awe raia wa Tanzania
- ii. Mwombaji awe na umri usiozidi miaka 45 na awe hajawahi kupatikana na kosa la jinai au kufungwa jela.
- iii. Maombi yote yaambatanishwe na maelezo binafsi yanayojitosheleza (Detailed CV).

- iv. Maombi yote yaambatanishwe na nakala za vyeti vya taaluma, vyeti vya elimu (IV au VI), cheti cha kuzaliwa na picha mbili za rangi za hivi karibuni (passport size) ziandikwe jina la mwombaji nyuma.
- v. Testimonials Provisional results "Statement of results" hati ya matokeo ya kidato cha nne na sita HAVITAKUBALIWA.
- vi. Waombaji watakaowasilisha taarifa na sifa za kughushi watachukuliwa hatua za Kisheria.

Maombi yatumwe kwa:-

MKURUGENZI MTENDAJI,
HALMASHAURI YA WILAYA,
S.L.P.83,
KALIUA.

Tarehe ya mwisho ya kupokea maombi ni tarehe 30/11/2021 saa 9.30 mchana.


J. D. Mwaga

Mkurugenzi Mtendaji Wilaya

MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA KALIUA
S.L.P. 83
KALIUA